# Twende Pamoja
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

Toleo maalum la kampeni ya afya na usafi wa mazingira Mei 2018 002

NDANI



Shule za Msingi zinavyotekeleza kampeni ya Usafi wa Mazingira

UK. 04



Habari katika Picha

Uk 19&20

## Sovi, Image vijiji vya mfano kitaifa kampeni ya Usafi wa Mazingira

" Sasa kuhamia Digitali kwa kishindo Muda wowote"



*Mkuu wa Wilaya ya Njombe Bi Ruth Msafiri(kulia) akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Bi Monica Kwiluhya funguo za gari na pikipiki baada ya Halmashauri yake kufanya vizuri kwenye mashindano ya kampeni ya afya na usafi wa mazingira Kitaifa na kupewa zawadi*

### Yaliyomo



Vijiji vya Sovi, Image kuachana na vibuyu chirizi

<< 12



Kampeni ya afya,usafi wa mzingira yatokomeza magonjwa Njombe

<< 05

## Ijue Kampeni ya Afya,Usafi wa Mazingira katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe

Kampeni ya Kitaifa ya afya na usafi wa mazingira nchini Tanzania ilizinduliwa na Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete mwaka , 2012 mjini Moshi Mkoani Kilimanjaro.

Kampeni hii ililenga kuinua kiwango cha upatikanaji wa huduma bora za usafi wa mazingira kwa kuinua uwiano wa kaya zenye vyoo bora kwa zaidi ya asilimia 50% hadi

>>> 03

# TAHARIRI

Karibuni Wasomaji wetu katika Toleo maalumu la Jarida la Twende Pamoja ambalo linakuletea namna kampeni ya afya na usafi wa mazingira inavyotekelezwa katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Toleo hili limejikita katika kuangalia mafaniko yaliyopatikana kupitia utekelezaji wa kampeni ya usafi wa mazingira katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe. Mafaniko haya yameakisiwa zaidi katika vijiji vya Sovi na Image ambavyo ni vijiji vilivyofanya vizuri katika kampeni hii.

Moja ya mafanikio ya kampeni katika vijiji hivi nikuwezasha kuepukana na magonjwa ya mlipuko hivyo wananchi kutumia muda mwingi kwenye uzalishaji mali kuliko kutafuta matibabu.

Sambamba na hilo kampeni hii imefanikiwa sana katika upande wa shule za Msingi kwenye vijiji hivi ikiwemo kuongeza kiwango cha ufaulu kwenye shule za Msingi kutokana na mazingira mazuri na rafiki ya kujifunzia na kufundishia.

Ni imani yetu kuwa kupitia toleo hili wananchi wa Njombe na Tanzania kwa ujumla watajifunza mambo mengi muhimu kuhusu umuhimu wa kampeni ya afya na usafi wa mazingira ili kuondokana na matatizo mbalimbali ambayo yanaleta gharama kubwa katika kuyatatua pamoja na kupoteza nguvu kazi ya taifa.

Shukrani za pekee ziwaendee wadau wote wa maji na usafi wa mazingira ambao tumekuwa tukishirikiana katika kampeni hii.

Tunawatakia usomaji Mwema.

Twende pamoja.

Jarida hili Hutolewa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

S.L.P 547
NJOMBE

Simu: 026 2782111

Fax: 026 2782857

Email:ded@njombedc.go.tz

info@njombedc.go.tz

njombedc@yahoo.com

Tovuti:www.njombedc.go.tz

## BODI YA UHARIRI

MONICA PZ KWILUHYA-
MKURUGENZI MTENDAJI

LUKELO MSHAURA-
MHARIRI MKUU

REMIGIUS SUNGU
-MHARIRI

PETER MKILAMWENE
MHARIRI

MSANIFU KURASA
LUKELO MSHAURA.

JIPATIE NAKALA YA JARIDAHILI KWA PAKUA KWENYE TOVUTI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE www.njombedc.go.tz

## SERA YA UHARIRI

Madhumuni ya Jarida hili ni kuhabarisha na kuelimisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Halmashauri ya wilaya ya Njombe. Aidha Sera , mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inafafanuliwa kupitia Jarida hili . Isipokuwa pale itakapokatazwa habari za Jarida la Twende Pamoja zinaweza kunukuliwa mradi Mhariri ajulishwa kwa maandishi.

# Kampeni ya Afya na Usafi wa Mazingira Halmashauri ya Wilaya ya Njombe

<<< 01






*Kushoto ni choo cha zamani cha Shule ya Msingi Iditima kabla ya ujenzi wa choo bora kupitia Kampeni ya afya na usafi wa Mazingira. Kulia ni choo kipya cha shule ya Msingi Iditima baada ya kampeni ambapo kimezingatia mahitaji muhimu kwa walemavu pamoja na chumba kwa ajili ya wasichana waliopevuka.*

hadi kufikia mwaka 2015.

Kampeni hii ililenga kupunguza kuenea kwa magonjwa yasababishwayo na mazingira machafu (Sanitation related diseases).

Awamu ya kwanza imetekelezwa katika ngazi ya kaya na katika shule za msingi na ililenga kuhakikisha kuwa kila kaya katika eneo la kampeni inakuwa na vyoo bora pamoja na miundombinu ya kunawa mikono baada ya kutoka chooni.

Ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kampeni hii inatekelezwa katika kata zote 12, vijiji 45 na vitongoji 227. Pamoja na kutekelezwa katika shue 52 za msingi zilizoko katika Halmashauri.

Katika ngazi ya jamii na kaya mambo mbalimbali yamefanyika ili kuweza kufanikisha kampeni hii ikiwemo kutoa mafunzo kwa viongozi wa Halmashauri (Wajumbe wa baraza la ushauri la wilaya (DCC), Baraza la madiwani, wakuu wa Idara na vitengo pamoja na wadau mbalimbali waliopo katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Kutoa mafunzo kwa timu ya usimamizi wa kampeni ngazi ya Wilaya ikijumuisha wataalam kutoka idara ya Afya, maji, elimu msingi na maendeleo ya Jamii.

Ili kuweza kufanikisha kampeni ,Halmashauri ilitoa mafunzo ya utekelezaji wa kampeni kwa viongozi wa kata,vijiji na vitongoji vyote pamoja na wahudumu wa afya katika vijiji vyote vya kampeni pamoja na kukusanya takwimu za usafi wamazingira na kuziingiza katika rejista maalum za kitongoji.

Aidha, mikutano ya uhamasishaji (uchefuaji) ilifanyika katika vitongoji vyote 227 vilivyopo katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Kutokana na kampeni hii kuhusisha Nyanja mbalimbali mafunzo yalitolewa kwa mafundi ujenzi juu ya ujenzi wa vyoo bora ili kuhakikisha ujenzi wa vyoo unazingatia kanuni zote za afya na usafi wa mazingira.

Sambamba na hayo ufuatiliaji wa mara kwa mara ulifanyika ili kuona maendeleo ya utekelezaji wa kampeni pamoja na kufanya vikao mbalimbali vya tathmini ya utekelezaji na kubadilishana uzoefu kati ya viongozi wa vitongoji, vijiji, kata, Wilaya na wadau mbalimbali wa usafi wa mazingira katika Halmashauri jambo lililochangia mafanikio makubwa kwenye usafi.



*Ujenzi wa vyoo bora kwenye shule za Msingi unakwenda sambamba na ujenzi wa miundombinu ya kunawia mikono*

# Kampeni ya afya na usafi wa mazingira kichocheo cha ufaulu shule ya Msingi Image

Unapofika katika kijiji cha Image ambacho ni miongoni mwa vijiji vya mfano Tanzania katika utekelezaji wa kampeni ya afya na usafi wa mazingira, moja ya kivutio kikubwa ambacho ni utunzaji wa mazingira ni shule ya Msingi Image.

Mbali na kuwepo na ndoo za kuzolea uchafu karibu kila baada ya mita kadhaa, shule hii imezungukwa na mabango yenye ujumbe wa aina mbalimbali unaosisitiza elimu na usafi wa mazingira.

Shule ya Msingi Image ambayo ilianzishwa mwaka 1974 mbali ya kuwa na vyoo bora vilivyozingatia mahitaji maalumu kwa walemavu na wasichana waliopevuka, inamiundombinu ya kunawia mikono baada ya kutoka chooni.

Shule hii ni miongoni mwa shule za msingi zinazotekeleza kampeni ya afya na usafi wa mazingira kupitia shirika la UNICEF pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Kupitia kampeni ya afya na usafi wa mazingira, kiwango cha ufaulu kimeongezeka kutokana na kuwepo kwa mazingira rafiki ya kujifunzia na kufundishia.

Kwa mujibu wa mkuu wa shule ya Image, Shadrack Sodike anasema kabla ya kampeni ya afya na usafi wa mazingira kiwango cha ufaulu kilikuwa kidogo kuliko sasa.

Anasema kampeni ya usafi wa mazingira imewezesha ujenzi wa vyoo bora jambo ambalo limechochea wanafunzi wengi kufika shuleni hususani wasichana kutokana na kutokuogopa na kuwepo na mazingira mazuri ya kuwasitiri hivyo kupata muda wa kusoma zaidi wa kujifunza tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

" Awali wanafunzi wa kike waliopevuka kila mwezi walikuwa wanakosa masomo wakati mwingine hadi wiki moja jambo lililochangia kuathili maendeleo yao kitaaluma,hii ilitokana na miundombinu kutokuwa rafiki hivyo kulazimika kushinda nyumbani, Sasa hakuna mwanafunzi wa kike anayekosa masomo kutokana na vyoo bora vilivyozingatia mahitaji yao ya kibaiolojia" anabainisha Sodike

" Kiwango cha ufaulu kimeongeza ambapo toka mwaka 2014 hatujawahi kushuka chini ya asilimia 80 huku mwaka 2015 na 2016 ufaulu ukiwa kwa asilimia 100" alisema Sodike.

"Hapa tuna programu ya usafi wa mazingira shuleni (SWASH) wanafunzi wana kikundi chao ambacho kazi yake ni kutoa elimu kuhusu afya na usafi wa mazingira kwa wanafunzi wenzao kwa njia mbalimbali za nyimbo, ngojera na maigizo" alisema Sodike.

Unapokwenda kwenye vyoo vya shule hii ambavyo ni vya sinki huku sakafu yake ni marumaru unakutana na bango lenye ujumbe unaomkumbusha mwanafunzi nini anatakiwa kufanya kabla na baada ya kutoka chooni.

Kwa kuwa wanafunzi wanakula chakula cha mchana shuleni, kimetengwa chumba maalumu kwa ajili ya kuhifadhi maji safi na salama ili kulinda afya za wanafunzi.

Kampeni ya afya na usafi wa mazingira imeleta manufaa makubwa kwa wanafunzi wa Image.



*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Image iliyopo katika wakichota maji kwa ajili ya kunawa mikono kabla ya kupata chakula cha Mchana.Ujenzi wa vyoo bora umekwenda sambamba na ujenzi wa miundombinu ya maji kwenye shule za Msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.*

# Kampeni ya Afya na usafi wa mazingira yatokomeza Magonjwa Kijiji cha Image Njombe.

Kijiji cha Image ni kijiji kinachopatikana Kata ya Kidegembye iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Kijiji hiki kina Zahanati moja ambayo inahudumia jumla ya vitongoji 6 vyenye wakazi takribani 4342.

Kabla ya kuanza kwa kampeni ya afya na usafi wa mazingira katika kijiji hiki zahanati hii ilikuwa inapokea wagonjwa wengi wa magonjwa ya kuambukiza kama kuharisha, minyoo, na magonjwa ya ngozi kwa wastani wa wagonjwa 10 kwa wiki.

Kufuatia hali hiyo ililazimika kuwa na dawa nyingi za magonjwa hayo ili kuweza kukabiliana na hali iliyopo jambo ambalo lilikuwa linahitaji fedha nyingi katika ununuzi wa madawa.

Magonjwa yaliyokuwa yanashika nafasi tatu kwa kupatikana kwa wingi katika kijiji hiki yalikuwa yale yanayosababishwa na uchafu.

Baada ya kuanza kwa kampeni ya Afya na usafi wa mazingira viongozi wa kijiji wakishirikiana na wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe walikaa na kuweka mipango thabiti ya kutokomeza magonjwa hayo.

Tangu kampeni ya usafi wa mazingira ilipoanza wananchi wamekuwa na muitikio chanya juu ya usafi wa mazingira na mwili ili kuboresha afya na kutokomeza maambukizi ya magonjwa yanayotokana na uchafu.

Elimu inatolewa katika mazingira mbalimbali ikishirikisha viongozi wa vijiji, vitongoji na wataalamu wa afya kutoka zahanati ya Image zikiwemo kamati za afya .



*Bi Sara Chambachamba Afisa Maendeleo ya Jamii akiwaelekeza viongozi wa Vitongoji vya kijiji cha Image namna ya unawaji mikono ikiwa ni sehemu ya mafunzo kwenye Kampeni ya Afya na Usafi wa Mazingira wilayani Njombe.*

> " Kutoka wagonjwa 10 kwa wiki hadi kufikia mmoja na wakati mwingine hakuna kwa Mwezi"

Kampeni ya ujenzi wa vyoo bora imetoa matunda mazuri kwa wananchi na kupunguza magonjwa ya kuambukiza yanayotokana na uchafu.

Moja ya mafanikio makubwa ya kampeni hii ni Kupungua kwa magonjwa ya kuambukiza kama kuharisha, minyoo.

Kwa mujibu wa Mganga mfawidhi wa Zahanati ya Image ,Ayubu Mwasamengo anasema kwa sasa idadi ya wagonjwa wanaoletwa katika Zahanati hiyo ambao magonjwa yao yanasababishwa na uchafu imepungua kutoka wagonjwa 10 kwa wiki hadi kufikia wagonjwa wawili au mmoja na wakati mwingine hakuna kabisa kwa mwezi mzima

" Zamani ungekuja hapa zahanati ungeona tulikuwa na idadi kubwa sana ya wagonjwa wa minyoo, tumbo, ata ukiangalia ubao wa magonjwa yanayoongoza katika kijiji hiki nafasi 3 za juu hakuna ugonjwa unaotokana na uchafu" alisema Mwasamengo.

Anaeleza kuwa elimu iliyotolewa kwa wananchi kupitia kampeni ya afya na usafi wa mazingira imesaidia sana kutokomeza magonjwa yatokanayo na uchafu.


"Mbali ya kutoa matibabu nilikuwa natoa elimu , viongozi wa vijiji na vitongoji walikuwa wananialika kwenye mikutano ya hadhara ya vijiji na wataalamu wenzangu kwenda kutoa elimu, tunashukuru mwitikio mzuri wa wananchi na sasa jamii ya Image iko salama" alisema Mwasamengo

# Wasemavyo wana Image kuhusu Ujenzi wa Vyoo Bora Njombe.



**Eliza Ngoda.**
**Mkazi wa Kijiji cha Image**

Nilipopata elimu tu nikaanza kujenga choo,tangu Nimejenga Choo cha Sinki Mimi na familia yangu tumekuwa Salama kabisa na hasa baada ya kuanza kuzingatia matumizi sahihi ya vyoo. Zamani Magonjwa ya kuhara na tumbo yalikuwa yanaisumbua sana familia yangu pia harufu ilikuwa kali sana lakini sasa mambo ni mazuri. Nilianza kujenga choo kidogo kidogo kwa kununua bomba la kutolea hewa baadae sinki, simenti na mwisho nikanunua bati na kuezeka choo changu



Romanus Scopion Mnywele (52)
Mwenyekiti Kijiji
cha Image.

Toka tumehamasishwa na serikali na sisi tukawaamasisha watu na mwitikio ulikuwa mzuri. Kampeni tulianza mwaka 2014 hadi sasa 2018 watu hawapingi ujenzi wa vyoo bora ambao unamanufaa makubwa sana kwetu. Wanachohitaji wananchi ni elimu tu basi wakielimishwa wanaelewa na .kutekeleza

Ujenzi wa vyoo hivi bora umekuwa na mafanikio makubwa katika Nyanja mbalimbali hususani elimu. Mahudhurio shuleni kwa wanafunzi ni mazuri, nyumbani kuna choo bora na shuleni choo bora hali inayomvutia mwanafunzi kwenda shuleni tofauti na hapo awali ambapo shuleni .pekee kulikuwa na vyoo bora

Napenda kutoa wito kwa watanzania kujenga vyoo bora ili kuliepusha taifa kuingia katika gharama kubwa kwa ajili ya madawa ya kutibu magonjwa , ya kuhara na tumbo ambapo kama tukiwa na vyoo bora fedha hizo zinaweza kutumika katika mambo mengi ya maendeleo .Taifa letu



Romanus Scopion Mnywele (52)
Mwenyekiti Kijiji

# Kampeni ya Afya na Usafi wa Mazingira Kijiji cha Image



**ISRAEL FEDSON MHADA (Mwenyekiti Kitongoji cha Mlangali)**

Awali wananchi walikuwa na vyoo vya mabanzi na idadi kubwa walijisaidia vichakani nyakati za usiku kutokana na vyoo kutowasitili wakati wa mchana, magonjwa yalikuwa mengi lakini sasa watu wanavyoo bora na magonjwa yamekwisha kabisa katika kitongoji changu. Asante serikali kwa kutupa elimu na kutupunguzia gharama ..za matibabu kupitia kampeni ya Usafi wa Mazingira



**ELINA LULAMSO MWADA (50)**

Gharama za ujenzi wa vyoo bora na utunzaji wa mazingira ni ndogo kuliko matibabu ya mtu anayeugua kipindupindu au magonjwa mengine yatokanayo na uchafu .Tujitahidi kuweka mazingira yetu katika hali ya usafi ili kuwalinda watoto na jamii inayotuzunguka. Sisi hapa Image tumeweza na ndio maana tunashika nafazi za juu kitaifa katika mashindano ya afya na usafi wa mazingira.Mwananchi .akiamua anaweza, usafi ndio kila kitu kwetu tumeona faida zake




**Ludaliko Kitango - Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mtoho Kijiji cha Image**

Tumehamasishwa na kupewa elimu na wataalamu wa Halmashauri na sisi tukaenda kutoa elimu kwa wananchi na mwitikio ukawa mzuri. Wananchi hawapingi kujenga vyoo bora wanachohitaji ni elimu na wakielimishwa wanaelewa na kutekeleza bila shida. Sisi elimu ndio imesaidia sana na ufuatiliaji wa mara kwa mara wa maazimio ya vikao kuhusu ujenzi wa vyoo bora kijijini kwetu.



**EMILIKO HOTMAN LUHEMA**

Tulianza uhamasishaji kwenye mikutano ya Kitongoji kila tunapofanya agenda ya usafi ilikuwepo, tuliendelea kuwahimiza wananchi hadi walipoacha vyoo vya mabanzi na kujenga vyoo vya tofali na vyenye masinki, mabomba ya kutolea uchafu, pamoja na vifaa vya kunawa mikono baada ya kutoka chooni. Wageni wakija kwenye kitongoji chetu wanapewa utaratibu wa kitongoji chetu kama anataka kujenga nyumba

# Wasemavyo Viongozi Kuhusu Mafanikio ya Kampeni ya Afya na Usafi wa Mazingira kijiji Sovi Kata ya Mtwango

SULEIMAN NZAMILISI: AFISA AFYA KATA YA MTWANGO.

Mafanikio makubwa tuliyopata kupitia kampeni hii ni watu kujenga choo kwa asilimia mia moja kwa kuzingatia vigezo vya kampeni ikiwemo choo cha sinki, bomba la kutolea harufu pamoja na miundombinu ya kunawia mikono baada ya kutoka chooni, Elimu tuliyotoa juu ya matumizi stahiki kwa sasa imekuwa tabia endelevu katika jamii na tunaimani itarithishwa vizazi na vizazi. Tumejenga jamii ya watu wastaarabu pamoja na kupunguza magonjwa yatokanayo na uchafu. Kwa sasa mkazo tumeweka kwenye kuhama kutoa matumizi ya vibuyu chirizi na kuingia matumizi ya ndoo ambapo hadi sasa katika kijiji cha Sovi matumizi ya ndoo ni asilimia 100.





SAMSON LYABONGA (52) MJUMBE WA KAMATI YA AFYA KIJIJI CHA SOVI



JAMES MNGINDO (30) MJUMBE WA KAMATI YA AFYA KIJIJI CHA SOVI



NOELY NDUNDURU MWENYEKITI WA WA KIJIJI CHA SOVI

"Tulipozungumza kwenye mkutano kuhusu kampeni hii tukaanza kutoza faini wale wote ambao hawakutekeleza, faini hizi tulizitumia kujenga vyoo vya wazee na wajane wasiojiweza, hatimaye kijiji kizima kikawa na vyoo bora na kupungua kwa magonjwa yanayotokana na uchafu kijijini kwetu"

"Ujenzi wa vyoo bora tulianza kwa hatua, mara ya kwanza vyoo vyetu vilikuwa vya nyasi na vimetengenezwa kwa mabanzi hali iliyokuwa inatishia usalama wetu pamoja na familia, baada ya kupewa elimu tukajenga vyoo vya sink tukaezeka na bati na tunatumia ndoo chirizi kunawa mikono."

"Uchafu ni uzembe maana unaleta maradhi mbalimbali kama magonjwa ya tumbo, kuhara. Tulipopewa elimu kutoka Halmashauri na sisi tukaileta elimu hi na kila kusanyiko tulihamasisha na kutoa elimu hatimaye tumefanikiwa, Tunawashukuru wananchi wa Sovi kwa ushirikiano"

# Wasemavyo Viongozi Kuhusu Mafanikio ya Kampeni ya Afya na Usafi wa Mazingira kijiji cha Image

Moja kati ya watu wa muhimu waliofanikisha kampeni ya afya na usafi wa mazingira katika Kijiji cha Image wilayani Njombe ni viongozi kuanzia ngazi za vitongoji na vijiji ambao wamefanya kazi bega kwa bega katika kuhamasisha na kutoe elimu juu ya umuhimu wa ujenzi wa vyoo bora na usafi wa mazingira.



SHADRACK SODIKE
MWALIMU MKUU SHULE YA MSINGI IMAGE

"Kampeni ya afya na Usafi wa Mazingira imewezesha shule yangu kuwa na vyoo bora pamoja na miundombinu ya kunawia mikono, maudhurio ya wanafunzi yamekuwa mazuri na ufaulu umeongezeka kutokana na mazingira Bora hapa Shuleni. Tunaishukuru Sana Serikali Kupitia Halmashauri na wafadhili"



AYUBU MWASAMENGO
MGANGA MFAWIDHI ZAHANATI YA IMAGE

"Kwa sasa inaweza kupita ata wiki mbili bila kupokea mgonjwa wa magonjwa ya tumbo, kuhara au amiba, kampeni ya afya na usafi wa mazingira imesaidia tofauti na awali ambapo nilipokea wagonjwa kuanzia 10 kwa wiki wakiumwa magonjwa ya kuhara, ngozi na mengine mengi yasababishwayo na uchafu"



RONICA KOLIMBA
AFISA MTENDAJI WA KIJIJI CHA IMAGE

"Watu wasiotekeleza kampeni huwa tunawaelimisha baada ya hapo akikaidi tunatumia sheria ndogo za kijiji. Suala la usafi wa mazingira ni agenda ya kudumu katika mikutano yetu ya kijiji ndio maana uelewa wa wananchi ni mkubwa kuhusu masuala ya usafi"

JULIUS SALINGWA: DIWANI WA KATA YA KIDEGEMBYE

*Baada ya kufanya vizuri Shule za Msingi kata yangu imejipanga pia kwenye shule ya Sekondari, kazi ya awali ilikuwa kuweka vyoo bora ambayo imekamilika sasa ni kuendelea kuboresha.Nataka kwenye Kata yangu iwe ya mfano , mtoto awe anaanzia nyumbani kukuta vyoo bora, kisha anaingia darasa la awali, Shule ya Msingi na hatimaye shule ya Sekondari. Kampeni ya afya na usafi wa mazingira inafaida kubwa maana magonjwa kwa sasa hakuna watu wangu wanatumia muda mwingi kwenye uzalishaji mali na kuinua kipato cha familia. Tumeamua na Tumeweza.*



WAJIBU WA KAMATI ZA WASH KATIKA SHULE ZA MSINGI ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

1) Kuwafundisha wanachama na wanafunzi wengine masuala ya maji na usafi wa mazingira
2) Kuwafahamisha wanajamii wa shule kufanya usafi, kupanda miti na kazi zingine nzuri.
3) Kukagua pointi za maji, vyoo, unawaji mikono na mazingira kwa ujumla.
4) Kutengeneza program za kukusanya pesa ili kuwa na mfuko ili kuwa na mfuko maalumu wa kununua vifaa vya usafi.
5) Kutengeneza program mbalimbali na kuzifikisha katika jamii. program hizo zinaweza kuhusiana na:

- Kampeni ya usafi wa mazingira.
- Kusafisha vyanzo vya maji
- Kuvilinda vyanzo vya maji kutokana na mafuriko, wanyama n.k

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kuna jumla ya shule za msingi 52 ambapo jumla ya shule 48 sawa na asilimia 92% zimefanikiwa kuwa na klab hizi. Jitihada za kuhakikisha kuwa shule zote zinakuwa na klabu hii zinaendele kufanyika.

# Kampeni ya Usafi wa Mazingira kuongeza uzalishaji mali Njombe

Kutekelezwa kwa ufanisi kwa kampeni ya afya na usafi wa mazingira katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe , kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na utashi wa wananchi na jitihada za viongozi katika kutoa elimu na kuihamasisha jamii.

Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Monica PZ kwiluhya anabainisha kuwa kampeni ya afya na usafi wa mazingira imefanikiwa sana katika kaya na jamii kutokana na usimamizi thabiti pamoja na elimu iliyotolewa kwa wananchi.

Anabainisha kuwa mbali na kampeni kusaidia jamii kuepukana na magonywa yatokanayo na uchafu, Halmashauri yake imefaidika kwa kupata vitendea kazi ambavyo vinasaidia katika utekelezaji wa shughuli za afya na usafi wa Mazingira.

Vitendea kazi hivyo vimetolewa na Wizara baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kufanya vizuri kwenye kampeni ya afya na usafi wa mazingira

"Kufanya vizuri kwenye kampeni Kitaifa kumewezesha Halmashauri kupata zawadi za vitendea kazi ambavyo ni gari na pikipiki kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa kampeni hii, vifaa hivi vinatusaidia sana kufika maeneo mbalimbali kutoa elimu pamoja na kufanya



*Monica Kwiluhya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe.*

ufuatiliaji kwenye Kata na vijiji vyetu." Alisema Kwiluhya.

"Sisi kama viongozi kazi yetu ni kuwajengea msingi mzuri wananchi na kuhakikisha wanaelewa kile ambacho serikali inapanga kufanya" alibainisha Kwiluhya

"Tunaendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya usafi wa mazingira kuanzia ngazi ya kaya, taasisi za umma na watu binafsi ili kuendelea kuiweka jamii yetu salama na kuogeza uzalishaji ambao utasaidia maendeleo ya Halmashauri na taifa kwa ujumla" aliongeza Kwiluhya.

Anasema kuwa mwanzoni mwa utekelezaji wa kampeni baadhi ya wananchi walikuwa wagumu kuelewa lakini baada ya elimu pamoja na usimamizi thabiti walielewa na kufanya vizuri kwenye kazi zao.

"Tunahakikisha shule zetu za msingi zinakuwa bora kwa kutengeneza vyoo bora na vya kisasa ambavyo vinazingatia mahitaji muhimu ya walemavu, miundombinu ya kunawa mikono pamoja na chumba maalum cha kuwasitiri wanafunzi waliopevuka" wanapokuwa kwenye hedhi".

# Klabu za Usafi na Mazingira Shuleni (School Wash Clubs) kichocheo cha Mabadiliko Njombe

Katika kutekeleza kampeni ya afya na usafi wa mazingira shuleni kupitia program ya usafi wa mazingira shuleni ( SWASH) Halmashauri ya wilaya ya Njombe imekuwa ikitoa mafunzo mbalimbali na namna shughuli za klabu hizo zinavyotakiwa kufanyika.

Hatua hii imeleta mafanikio makubwa katika utekelezaji wa kampeni ya afya na usafi wa mazingira na kuwa kichocheo kikubwa cha mabadiliko katika jamii kuhusu mtizamo wa usafi na mazingira.

Klabu za SWASH kwenye shule zinamajukumu mbalimbali ikiwemo kuhakikisha kuwa mazingira ya shule yanakuwa safi wakati wote. Klabu hizi hutumia njia ya mtoto kwa mtoto kufikisha elimu mbalimbali ya afya na kupunguza magonjwa yanayosababishwa na uchafu wa mazingira



*Mwalimu wa klabu ya usafi wa mazingira Shuleni (Swash) Amiry Mtokoma wa shule ya Msingi Sovi akiwafundisha wanafunzi namna bora ya kunawa baada ya kutoka chooni ili kujikinga na maradhi*

### MALENGO YA MAFUNZO YA SWASH

1) Kumjenga mtoto katika tabia nzuri za usafi
2) Kutoa ujumbe wa afya katika jamiii kupitia watoto wa shule kwa mabadiliko
3) Kuwasaidia watoto kujenga na kuwa na furaha na kujifunza vizuri
4) Kuongeza uelewa wa wafanyakazi wa afya katika jamii na uhusiano na watoto wa shule



*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Image ambao ni Klabu ya SWASH wakiwa katika moja ya majukumu yao ambayo nikuelimisha wanafunzi wenzao kuhusu afya na usafi wa mazingira shuleni*

### VIPENGELE VINAVYOZINGATIWA KATIKA MAFUNZO YA SWASH KWA WANAFUNZI KATIKA SHULE ZA MSINGI

- Maji safi na salama
- Usafi binafsi
- Uandaaji na utunzaji salama wa chakula na ulaji salama
- Usafi wa Mazingira kwa
- ujumla
- Matumizi sahihi ya vyoo katika shule na katika jamii

# Mafanikio ya kampeni ya usafi wa mazingira katika vijiji vya Sovi na Image.

Vijiji vya image na Sovi ni miongoni mwa vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe vilivyotekeleza kwa mafanikio makubwa kampeni ya kitaifa ya Usafi wa Mazingira.

Kampeni hii ililenga kuinua kiwango cha upatikanaji wa huduma bora za usafi wa mazingira kwa kuhakikisha kuinua kiwango cha kaya zenye vyoo bora kwa asilimia 100% ndani ya kipindi cha miaka miwili.

Katika vijiji hivi kaya zote zimejenga vyoo bora vyenye sinki na bomba maalum la kutolea hewa pamoja na kuwa na miundombinu ya unawaji mikono mara baada ya kutoka chooni.

Vijiji hivi vyote vimethibitishwa na wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia wazee na watoto kuwa ni vijiji bora daraja la kwanza (ODF villages level I).



*Afisa afya wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe, Remigius Sungu akiwa ofisini kwake*

# Nini kilipelekea mafanikio haya?

Afisa afya wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe Bw. Remigius Sungu anabainisha mambo yaliyopelekea mafanikio Katika utekelezaji wa kampeni ya usafi kama ifuatavyo:-

Kutoa mafunzo ya utekelezaji wa kampeni ya usafi wa mazingira kwa viongozi vijiji na vitongoji vyote pamoja na wahudumu wa afya katika kila kijiji.

Kukusanya takwimu za usafi wa mazingira na kuziingiza katika rejista maalum za kitongoji kwa vijiji vyote

Kufanya mikutano ya uhamasishaji (uchefuaji) katika vitongoji vyote 6 vya kijiji cha Image na vitongoji 3 vya kijiji cha Sovi.

Kutoa mafunzo kwa mafundi ujenzi juu ya ujenzi wa vyoo bora ambapo katika kijiji cha Image jumla ya mafundi 5 walipata mafunzo na kijiji cha sovi mafundi 3 walipata mafunzo

Kuunda kamati maalumu za usafi wa mazingira katika kila kijiji. Kamati hizo zilijumuisha viongozi wa kijiji (Mtendaji na Mwenyekiti), viongozi wa vitongoji vyote, wahudumu wa afya ya msingi wa kijiji, viongozi wa dini pamoja na wajumbe wachache waliopendekezwa na wananchi wakati wa mikutano ya uchefuaji. Kamati hii imehusika moja kwa moja kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuhakikisha kila kaya inatekeleza kampeni hii.

Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa wataalam kutoka ngazi ya wilaya ili kuona maendeleo ya utekelezaji wa kampeni hii na kutatua changamoto mbalimbali zinazozuia utekelezaji.

Kufanya vikao mbalimbali vya tathmini ya utekelezaji na kubadilishana uzoefu katika ngazi ya kijiji ambapo kila robo mwaka timu ya usimamizi wa kampeni ngazi ya Halmashauri hukutana na kamati ya usafi wa mazingira

>> 15

# Usafi wa mzingira kwetu ni kipaumbele- Msafiri



*Mkuu wa Wilaya ya Njombe Bi Ruth Msafiri akinawa katika kibuyu chirizi kwenye nyumba ya Mwananchi katika Kata ya Mtwango wakati akifanya ukaguzi wa utekelezaji wa kampeni ya afya na Usafi wa Mazingira*

"Tumeweza kushinda kitaifa katika masuala ya afya na usafi wa mazingira mfululizo hii inaonyesha kuwa hatubahatishi, tumedhamilia kufanya vizuri katika masuala ya afya na usafi wa mzingira katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe na wilaya kiujumla"

Hayo yalikuwa maneno ya Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Bi Ruth Msafiri wakati akiongea na jarida hili kuhusu mafanikio ya kampeni ya afya na usafi wa mazingira.

Anasema kuwa mafanikio katika nyanja ya afya na usafi wa mazingira yametokana na ushirikiano uliopo baina ya viongozi na wananchi ambao wameikubali na kuifanya kuwa endelevu katika maeneo yao.

"Siri ya mafanikio yetu ni elimu iliyotolewa kwa wananchi, ushirikishwaji na ufuatiliaji. Unaweza kuwapa wananchi elimu na mafunzo kama ujaweka mpango kazi na utaratibu mzuri wa kutekeleza, kufanya ufuatiliaji ikiwemo kuwashirikisha wananchi uwezekano wa kufanya vizuri ni mdogo jambo ambalo sisi kama wilaya tumefanikiwa" anaeleza Bi Msafiri.

Anaongeza kuwa ushirikishwaji wa wananchi umesaidia kugundua changamoto mbalimbali ambazo zimefanyiwa kazi na hatimaye kuibuka kinara katika usafi wa mazingira.

"Ukienda vijijini utakuta nyumba ya kawaida lakini ukienda kwenye choo ni kisafi, kizuri na kimejengwa kwa kufuata kanuni zote za afya ikiwemo kuweka vifaa vya kunawia mikono vya maji tiririka na wanafuata matumizi sahihi ya choo" anabainisha Bi Msafiri.

"Uzuri wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe hawasubiri mashindano katika suala la usafi kwani limekuwa ni agenda ya kudumu kwenye vikao kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiji, Kata na Halmashauri kwa Ujumla" anabainisha Bi Msafiri.

"Elimu hii imewaingia wananchi na sasa wanaona kuwa ni suala la kawaida katika maisha yao" anaongeza bi Msafiri.

Anaeleza kuwa Njombe hawalidhiki na kubweteka na mafanikio yaliyopatikana katika kampeni ya afya na usafi wa mazingira.

Tayari wameshaona faida ya kuwa na mazingira safi baada ya magonjwa kupungua na jamii kupata muda mwingi wa kufanya shughuli za uchumi jambo ambalo ni muhimu kufanikisha sera ya Tanzania ya Viwanda.

"Tunajivunia mafanikio yetu katika masuala ya usafi na mazingira, tunapenda tuendelee kuwa nayo na haturuhusu mtu atunyang'anye bali tunawaalika watu waje kujifunza nini tunachokifanya na kujifunza" aliongeza Bi Msafiri.

Anawapongeza wananchi wa Njombe kwa kuipokea na kutekeleza kwa vitendo kampeni ya afya na usafi wa mazingira na kutoa wito kwa wananchi wote kufanya suala la usafi kuwa tabia.

" Bila wananchi kuwa na mwitikio mzuri tusingefanikiwa , nawapongeza sana wananchi, viongozi na wadau mbalimbali wa mazingira kwa kuifanya Njombe kuwa kinara na nawakaribisha wageni waje kujifunza namna tunavyotekeleza kampeni ya afya na usafi wa mazingira"

# Mshikamano siri ya mafanikio ya usafi wa mazingira Halmashauri ya Wilaya ya Njombe

Mafanikio ya kampeni ya afya na usafi wa mazingira katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe yanatokana na mshikamano mzuri uliopo baina ya wataalam na viongozi wa siasa kuanzia ngazi ya Mkoa hadi Kijiji.

Baraza la madiwani limekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha kampeni hii kupitia uhamasishaji wanaoufanya katika mikutano mbalimbali ya maendeleo wanayoifanya na wananchi katika maeneo yao.

Hilo linathibitishwa na mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Valentino Aidan Hongoli, wakati akizungumza na waandaaji wa Jarida hili.

"Tulielimishwa kuhusu vinawia mikono, namna ya kuchimba mashimo ya taka, pamoja na kuwa na vichanja vya kuanikia vyombo badala ya kuanika chini, pia ulifanyika uchefuaji ,wananchi waliweza kuona ndio maana tumefanikiwa" alisema Hongoli

"Kila ninapopata nafasi ya kuongea na hadhara ya wananchi katika mikutano siwezi kuacha kuzungumzia suala la usafi wa mazingira kwa kuwa lina faida kubwa sana kwenye Halmashauri yangu, nimekuwa nikizungumza kupitia vikao vya baraza la madiwani, kwenye maadhimisho au kampeni mbalimbali za masuala mtambuka yanayofanyika katika Halmashauri yangu" Alisema Bw Hongoli.

"Kukosekana kwa choo kimoja katika jamii kunaweza kuleta madhara ya magonjwa ya kuambukiza kwa jamii nzima na hivyo kupunguza nguvu kazi ya Taifa" aliongeza Hongoli.

Bw Hongoli anasisitiza kuwa pamoja na jamii kuwa na vyoo bora kama vyoo hivyo havitatumika na kutunzwa vyema na kanuni za afya hazizingatiwi bado wataendelea kuandamwa na magonjwa kila siku.

Anabainisha kuwa ili kuweza kufanikisha kampeni ya afya na usafi wa mazingira lazima jamii iwe na umoja, mshikamano na izingatie sheria za afya na viongozi wazisimamie ipasavyo.

"Mfano mzuri kwenye Halmashauri yetu mbali na elimu tumejitungia wenyewe sheria ndogo ndogo ambazo tunazisimamia na kuhakikisha wanainchi wetu wanakuwa salama wakati huo tukiendelea kutoa elimu kwa wenzetu kupitia vyombo mbalimbali vya mawasiliano" alisema Hongoli.

"Vijiji vya Sovi na image vimefanikiwa kwa sababu kuna baadhi ya wanachi hawakuwa na uwezo wa kujenga bora, lakini kwa kuwa nia ilikuwa ni kuhakikisha jamii yao inakuwa salama basi waliwasaidia wale watu kufyatua tofali pamoja na ujenzi". alibainisha Hongoli

"Unapoongoza wananchi wenye afya bora basi kasi ya maendeleo huwa kubwa sana na hupatikana haraka" alibainisha Hongoli.

"Nawashukuru wananchi kwa kuipokea kampeni, kuchukua hatua na kuanza utekelezaji mara moja licha ya wachache kuanza kwa kusitasita, lakini mwishoni hao ndio walikuwa vinara wa kunadi mafanikio" alisema Hongoli.



*Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe, Valentino Aidan Hongoli akizungumza na wananchi wa Kata ya Mtwango wakati wa uzinduzi wa wiki la usafi wa mazingira katika wilaya ya Njombe.*

# << 12 Mafanikio ya Kampeni ya Afya

Kufanya vikao mbalimbali vya tathmini ya utekelezaji na kubadilishana uzoefu katika ngazi ya kijiji ambapo kila robo timu ya usimamizi wa kampeni ngazi ya Halmashauri hukutana na kamati ya usafi wa mazingira kuhusu mikakati ya kila kijiji kuhakikisha kampeni hii inafanikiwa.

Bw Sungu anaielezea mikakati hiyo kuwa ni pamoja na

-Agenda ya usafi wa mazingira kuwa ni agenda ya kudumu katika mikisanyiko na vikao vyote ndani ya kijiji.

-Kila kitongoji kuwa na ratiba maalumu ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa kampeni ya usafi wa mazingira mara moja kwa kila mwezi

-Kila kijiji kuitumia kila jumamosi ya mwisho ya mwezi kufuatilia utekelezaji wa kampeni ya usafi wa mazingira. Kamati ya usafi wa mazingira ya kijiji hutumia siku hii kufanya ukaguzi wa usafi wa mazingira kwa kila kaya

-Kila kijiji kuwa na sheria ndogo zinazosimamia utekelezaji wa kampeni hii ambapo wananchi wote wanaokiuka hupewa adhabu

-Wanufaika wa mradi wa kunusuru kaya maskini unaofadhiliwa na TASAF kutumia kiasi cha fedha wanachopata ili kuboresha vyoo na kuweka miundombinu ya unawaji wa mikono

- Vijiji kutumia faini zinazokusanywa kwa kusaidia kaya za wazee na yatima katika kuboresha hali za usafi wa mazingira katika kaya zao.

"Vijiji hivi vimekuwa ni vijiji vya mfano kitaifa katika utekelezaji wa kampeni hii, wageni kutoka maeneo mbalimbali Tanzania bara na visiwani wamekuwa wakifika kujifunza namna bora ya utekelezaji wa kampeni ya usafi wa mazingira. Tunawashukuru sana wadau mbalimbali wa maendeleo hasa UNICEF kwa ufadhili wao uliopelekea vijiji hivi kutekeleza kwa ufanisi program hii" anaeleza Bw Sungu.






*Picha upande wa Kushoto ni choo cha mwananchi Katika kijiji cha Sovi Kabla kampeni ya afya na usafi wa mazingira haijaanza katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe na kulia ni choo kilichojengwa baada ya Kampeni. Choo hiki ni cha sinki na kina miundombinu ya kunawia mikono pamoja na bomba la kutolea uchafu.*



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO
CHETI CHA UTHIBITISHO WA DARAJA LA UBORA WA USAFI
Hii ni kuthibitisha kwamba, Kijiji cha IMAGE Kata ya KIDEGEMBYE Halmashauri ya Wilaya ya NJOMBE, kimefikia hadhi ya kuwa na Vyoo bora kwa kila Kaya na hivyo kinatambuliwa kuwa ni Kijiji Bora DARAJA LA KWANZA
30-01-2018



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO
CHETI CHA UTHIBITISHO WA DARAJA LA UBORA WA USAFI
Hii ni kuthibitisha kwamba, Kijiji cha SOVI Kata ya MTWANGO Halmashauri ya Wilaya ya NJOMBE, kimefikia hadhi ya kuwa na Vyoo bora kwa kila Kaya na hivyo kinatambuliwa kuwa ni Kijiji Bora DARAJA LA KWANZA
30-01-2018
Dkt. Neema Rusibamayila
Tarehe

*Picha kushoto ni vyeti vya daraja la kwanza la ubora ambavyo vijiji vya Sovi na Image vimetunukiwa baada ya kufanya vizuri kati masuala ya afya na usafi wa mazingira*

# Uchefuaji mbinu shirikishi jamii iliyoleta mafanikio kampeni ya usafi wa mazingira Njombe.

Katikati ya mkutano mkuu wa Kijiji , wataalamu kutoka Halmashauri ya wilaya ya Njombe wanasimama na kuanza kutoa vifurushi walivyokuwa navyo.

Kila mmoja kwenye mkutano anaangalia kwa makini ni kitu gani hasa kinatolewa na hakuna ambaye anabaini mapema.

Mara kutoka kwenye moja ya vile vifurushi kinatolewa kinyesi cha binadamu mbele ya kadamnasi.

Ndio! kinyesi cha binadamu tena ambacho hakijakauka. Wananchi wanaanza kuona kinyaa na kulalamika. Kisha mtaalam kutoka Halmashauri anawaambia wananchi kwanini wanaona kinyaa wakati kila siku wanakula kinyeshi ndio maana magonjwa ya kuhara na tumbo hayaishi miongoni mwao.

Anawaeleza kinaga ubaga kuwa kinyeshi hicho wamekitoa mita chache tu kutoka katika maeneo wanayokaa na kimetapakaa karibu kila kona.

Ni kweli kulingana na mazingira ya Njombe na mwamko mkubwa wa wananchi katika upandaji wa miti , sehemu kubwa ni misitu au mazao hivyo ni lahisi kwa wananchi kujisaidia ovyo.

Mbinu hii inaitwa Uchefuaji yaani mbinu shirikishi jamii (CLTS).Mbinu hii ilitumika kuihamasisha jamii kuanzia ngazi ya vitongoji. Ni mbinu inayotia kinyaaa lakini yenye kuleta mafanikio.

Baada ya kupata elimu ya mbinu shirikishi jamii ya uchefuaji wananchi walihamasika na kuacha kujisaidia ovyo na kujenga vyoo bora na kuvitumia pamoja na miundombinu ya kunawia mikono kwa maji tiririka.

Mbali na kuhamasika ziliundwa kamati za usimamizi wa utekelezaji kampeni ya afya na usafi wa mazingira ngazi ya Kitongoji, kijiji na Kata. Kazi kubwa ya kamati hizi ilikuwa kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara .

Sambamba na hilo timu ya ufuatiliaji kutoka Halmashauri ya wilaya ya Njombe haikuwa nyuma katika kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara na kufanya vikao na kamati za vitongoji, vijiji na Kata ili kushirikiana kutatua changamoto wazazokutana nazo katika utekelezaji wa Kampeni.

Sasa vijiji vya Sovi na Image zina kaya zenye vyoo bora kwa asilimia 100 na miundombinu ya kunawia mikono.

Mazingira ya vijiji hivi kwa sasa ni safi na hakuna vinyesi vilivyotapakaa mitaani, mashambani pamoja na kwenye vichaka.

Ama kwa hakika uchefuaji kiboko!.

# Wasemavyo wanafunzi kuhusu Kampeni ya Afya na Usafi wa Mazingira Shule ya Msingi Sovi, Njombe



Faraja Mbangala
Mwanafunzi wa darasa la Saba shule ya Msingi Sovi

Kabla ya ujenzi wa vyoo bora katika shule yetu hali ilikuwa mbaya sana, mazingira yalikuwa machafu tulikuwa tunasita kwenda choo na wanafunzi wengi walikuwa wanaumwa magonjwa lakini toka tuanze kampeni tumeweza kuepukana na magonjwa hali ni Shwari.

Zamani tulikuwa tunaoona kinyaa kwenda chooni kutokan na uchafu na vyoo kutokuwa bora lakini sasa tunavyoo bora shuleni na ukirudi nyumbani pia tunavyoo bora tunaishi salama na kwa amani

*Johanetha Oscar Mgoba darasa la Sita shule ya Msingi Sovi*



# Vijiji vya Image na Sovi Kuachana na Vibuyu Chirizi wilayani Njombe



*Bi Joyce Mgoba mkazi wa kitongoji cha Sovi Kata ya Mtwango katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe akinawa mikono kwa sabuni baada ya kutoka kwenye choo*

Wakati kampeni ya Kitaifa ya afya na usafi wa mazingira inazinduliwa Tanzania na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa wakati huo Dr Jakaya Mrisho Kikwete, Juni 2012 mjini Moshi Mkoani Kilimanjaro kijiji cha Image na Sovi katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe havikuwa na vyoo bora.

Asilimia kubwa ya vyoo vilikuwa vya asili vilivyojengwa kwa mabanzi na hakukuwa na miundo mbinu yoyote ya kunawia mikono katika vyoo.

Kulingana na mazingira ya vijiji hivi hasa kijiji cha Image ambacho kina misitu mingi wananchi walipenda kujisaidia katika misitu pamoja na vichaka.

Hali hii ilipelekea wakazi wa vijiji hivi kuumwa magojwa mbalimbali ya matumbo na ngozi na kujikuta wanatumia muda mwingi kwenye matibabu kuliko kufanya shughuli za uzalishaji mali kutokana na mazingira kuwa machafu.

Mara baada ya kuzinduliwa kwa kampeni wataalamu wa afya kutoka katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe walikwenda kwenye Vijiji mbalimbali kutoa elimu juu ya umuhimu wa mazingira kuwa safi huku wakieleza malengo ya afya na usafi wa mazingira na nini Halmshauri inakusudia.

Kwa kutumia mbinu shirikishi jamii (CLTS) ambayo ilihusisha kutafuta vinyesi kwenye vichaka na kuwaonyesha kwa mfano kwenye mikutano ya uchefuaji jambo lililoleta kinyaa kwa wananchi na kuamua kubadilika.

Sambamba na hilo zilitungwa sheria ndogo ndogo za usafi wa mazingira ambazo zilikwenda sambamba na utozaji wa faini kwa wale waliokaidi.

Takribani miaka sita ( 6) imepita tangu kampeni hii imeanza, Ukifika katika vijiji hivi huwezi kukuta kinyesi kimezagaa wala huwezi kuona choo cha nyasi, nyumba zote zinavyoo vya masinki, mabomba ya kutolea hewa chafu pamoja na miundombinu ya kunawia mikono.

Mwanzoni mwa utekelezaji wa kampeni wananchi wengi walitumia vibuyu chirizi kama vifaa muhimu vya kunawia mikono mara baada ya kutoka chooni.

Vibuyu chirizi viliwekwa kwenye kila choo katika kijiji cha Sovi na Image na kusaidia kupunguza magonjwa yatokanayo na uchafu.

Baada ya kuona faida ya vyoo bora vyenye miundombinu ya kunawia mikino kwa sasa asilimia 100 ya wakazi wa vijiji vya Image na Sovi wanatumia ndoo chirizi na sio tena vibuyu chirizi.

Jambo la kuvutia kuna baadhi ya nyumba chache zimeezekwa kwa nyasi lakini vyoo vimeezekwa kwa bati huku kukiwa na vindoo vya kunawia mikono pamoja na sabuni.

Hii inaonyesha ni namna gani kampeni ya afya na usafi wa mazingira imefanikiwa kwenye Halmashauri ya wilaya ya Njombe

Wananchi wa vijiji hivi wanasema kwa sasa wamehamia "Digitali"

# Siri ya mafanikio ya usafi wa mazingira Kijiji cha Image Njombe.

Hadi kufanikiwa kufanya vizuri katika kampeni ya afya na usafi wa mazingira kuna vitu mbalimbali vilivyofanywa na viongozi katika kijiji cha Image. Ushirikiano wa pamoja baina ya wananchi na viongozi kwa kiasi kikubwa umekuwa chachu ya mafanikio hayo. Lakini malengo, sheria na taratibu kwa kiasi kikubwa ndio imekuwa chachu ya yote.

## Mpango Mkakati wa kuhakikisha kaya zote zinaendeleza kampeni ya afya na usafi wa Mazingira Image.

1.Kamati zote za afya ngazi ya vitongoji na vijiji zinafanya usafi wa mazingira kuwa agenda ya kudumu kwenye vikao
2.Kuhakikisha kila kila kaya inafanya usafi kwenye maeneo yake na ufuatiliaji kufanyika
3.Kuhakikisha kila kaya inakuwa na vifaa vya kufanyia usafi
4.Kutoa matangazo ya elimu ya afya na usafi wa mazingira katika maeneo ya kanisani, misibani, kwenye sherehe na kwenye mkusanyiko wa watu.
5.Viongozi wa kijiji kufanya ziara za mara kwa mara kukagua usafi wa mazingira kwenye kaya.
6.Kuhamasisha kila kaya kujenga choo ngazi ya D.




*Ofisi ya afisa Mtendaji wa Kijiji cha Image kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ambapo matangazo mbalimbali yanayohusu kampeni ya afya na usafi wa Mazingira yamebadikwa ukutani ili kumlahisishia mwananchi kukumbuka sheria na kanuni mbalimbali kuhusu usafi wa Mazingira*

## Sheria ndogo kijiji cha Image kuhakikisha kampeni ya afya na usafi wa mazingira inakuwa endelevu ambazo zimepitishwa na mkutano mkuu wa kijiji

1.Kaya isiyokuwa na choo faini tsh 50,000
2.Asiye na choo cha sink. 5000/=
3.Asiyeweka bomba la kutolea hewa tsh 5000/=
4.Asiyeweka maji ya kunawa ndani ya choo tsh 2000/=
5.Kinyesi kwenye choo cha sink 5000/=
6.Hana kibuyu chirizi tsh 2000/=
7.Kama hakuna mifagio 3000
8.Kaya kama haina shimo la kutupa taka 2500
9.Mazingira machafu kuzunguka kaya 5000
10.Sabuni ya kunawia kama hakuna chooni 1000
11.Mlango usiofungwa ndani na nje
12.Choo kuezekwa kwa paa la nyasi 5000
13.Sakafu isiyosafishika 3000

**KUMBUKA**

Lengo la Faini sio kumnyanyasa mwananchi bali ni kumkumbusha wajibu wake kuhusu usafi wa Mazingira



*Viongozi wa kijiji cha Image wakipewa maelezo namna kampeni ya afya na usafi wa Mazingira inavyotakiwa kutekelezwa ikiwa ni sehemu ya utoaji wa elimu. Ukutani ni matangazo mbalimbali yenye kuweka msisitizo suala la usafi wa mazingira kijiji cha Image Njombe.*



*Viongozi wa vijiji vya Image na Sovi wakiwa wakiwa na zawadi ya pikipiki na vyeti baada ya kufanya vizuri katika kampeni ya afya na usafi wa mazingira ngazi ya Taifa.*



*Miundombinu ya kunawa mikono baada ya kutoka chooni katika Shule ya Msingi Image imesaidia kupunguza magonjwa kwa wanafunzi kwenye shule hii*




*Vibao vyenye ujumbe wa kuhimiza usafi wa mazingira katika shule ya Msingi Image vimesaidia sana kuwakumbusha wanafunzi kuhusu kanuni za afya na usafi wa mazingira.*



*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Sovi wilayani Njombe wakinawa mikono baada ya kutoka chooni. Kampeni ya afya na Usafi wa mazingira imewezesha ujenzi wa vyoo bora pamoja na miundombinu ya kunawia mikono kwenye shule za Msingi katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.*



*Bi Rehema Ng'eve wa kijiji cha Sovi wilayani Njombe akinawa mikono baada ya kutoka chooni. Kwa sasa ameachana na kibuyu chirizi na kuamia kwenye ndoo baada ya kupata elimu kuhusu usafi wa mazingira*



*Afisa afya msaidizi Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ,Christopher Chongola akiwaelekeza watoto wa shule ya awali ya Patrick Momorial iliyopo kijiji cha Image namna ya kunawa kabla na baada ya kula. Elimu ya usafi hutolewa kuanzia ngazi ya Shule za awali ili kujenga tabia ya usafi wanafunzi*



*Mwalimu Amery Mtokoma wa Shule ya Msingi Sovi akielekeza kikundi cha SWASH cha Shule ya Msingi Sovi namna ya kunawa baada ya kutoka chooni. Vikundi vya Swach shuleni vimekuwa msaada mkubwa wa kutoe elimu kuhusu usafi wa mazingira*



*Afisa habari Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Lukelo Mshaura (kushoto) akiwa katika maandalizi ya utengenezaji wa vipindi vya redio, runinga na majarida kwa ajili ya kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kampeni ya afya na usafi wa mazingira wilayani Njombe*



*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Image wakifanya usafi wa mazingira katika shule yao ikiwa ni zoezi la kutekeleza wa Vitendo wa kampeni ya Afya na Usafi wa mazingira katika shule za Msingi*




*Picha ya gari pamoja na pikipiki ambazo ni zawadi ilizopata Halmashauri ya Wilaya ya Njombe baada ya kufanya vizuri katika mashindano ya afya na usafi wa mazingira Kitaifa.Kijiji cha Image ni miongoni wa vijiji vilivyofanya vizuri na kupelekea ushindi.*




*pichani ni moja ya vyoo bora katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe ambavyo vimezingatia mahitaji muhimu ya walemavu na wanafunzi waliopevuka. Vyoo hivi ni vya sinki na vina miundombinu ya kunawia mikono wanafunzi baada ya kutoka chooni.*